

## METHALI ZA KISWAHILI ZIHUSUZO ULEMAVU: MITAZAMO NA ATHARI ZAKE KATIKA JAMII

SHANI OMARI MCHEPANGE NA ELIZABETH GODWIN MAHENGE

---

Methali ni kipera muhimu cha fasihi simulizi katika kutoa mafunzo kutokana na maudhui yapatikanayo humo. Zimekuwa zikichukuliwa kuwa zina ukweli, hekima na busara kwa jamii husika. Lengo la makala hii ni kuzihakiki methali za Kiswahili ambazo zinahusu ulemavu ili kuelewa mitazamo iliyomo katika methali hizo na athari zake katika jamii. Maswali tunayojibu ni: Je, methali hizo zinabeba mitazamo gani ya jamii? Nini nafasi na athari ya mitazamo hiyo kwa maendeleo endelevu ya watu wenye ulemavu<sup>1</sup> na jamii husika? Data za makala hii zimekusanywa kupitia usomaji wa maandiko mbalimbali maktabani na kufanya mahojiano na wanajamii. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa, methali zimebeba mitazamo hasi na chanya kuhusu ulemavu na watu wenye ulemavu katika jamii. Aidha, methali hizo zinazungumzia mambo yanayohusu si tu ulemavu bali pia zinabeba mitazamo anuwai na falsafa ya Kiafrika kuhusu mambo mbalimbali katika jamii. Vilevile, imebainika kuwa methali hizo zinajenga na kuendeleza unyanyapaa na usaguzi kwa watu wenye ulemavu na hata makundi mengine katika jamii. Makala pia imebaini kuwa pamoja na ukweli kwamba methali zimekuwa chombo muhimu cha kupitishia falsafa na mafunzo mbalimbali kwa maendeleo ya jamii, baadhi ya methali hizo zinapaswa kufanyiwa marekebisha ili kuakisi mabadiliko ya kimtazamo na maendeleo mbalimbali katika wakati wa sasa.

---

**Keywords:** Swahili, methali, ulemavu

### Utangulizi

Dhana ya methali imefasiliwa na wataalamu mbalimbali. Mathalani, Mbiti anaeleza kuwa methali ni kanzi iliyosheheni imani, mawazo na busara za kijadi. Katika methali tunapata taarifa kuhusu dini na falsafa ya jamii mbalimbali za Kiafrika (Mbiti 2011). Aidha, methali ni semi fupifupi za kimapokeo zenye kuelezea fikra, maarifa, hekima na mafunzo yanayotokana na uzoefu wa jamii mahususi (Matei 2011). Katika jamii na tamaduni nyingi za Afrika, methali hutungwa hasa na wazee (watu wenye umri mkubwa) kwani wao ndio wanaonekana kuwa na sifa ya busara, ufahamu na tabia za kuigwa (Yankah 1999). Makala hii inachunguza mitazamo inayopatikana katika methali za Kiswahili zinazohusu ulemavu pamoja na athari zake kwa walemavu na jamii. Uhakiki wa methali hizi utasaidia kuelewa mitazamo ya jamii kupitia fasihi yao kuhusiana na ulemavu. Makala pia inalenga kuchochea tafakuri katika kujadili suala la ulemavu katika tanzu za fasihi na kuhimiza mipango ya kimaendeleo kuhusiana na watu wenye ulemavu nchini na katika jamii nyingine wazungumzazo Kiswahili Afrika Mashariki.

---

<sup>1</sup> Mlemavu na mtu mwenye ulemavu vimetumika kama visawe.

## METHALI ZA KISWAHILI ZIHUSUZO ULEMAVU

Ni vigumu kufasili ulemavu kwani unaweza kufasiliwa kwa vigezo kadhaa vikiwemo vya kitabibu na kijamii. Kwa mkabala wa kitabibu ulemavu unasababishwa na ugonjwa na matatizo ambayo humfanya mtu kupata changamoto za kijamii (Thomas 2004). Kwa mkabala wa kijamii, ulemavu ni mwingiliano kati ya matatizo katika viungo vya mwili na mazingira ya kiutamaduni-jamii (Quayson 2003) katika (Olaiya 2013. Vilevile, Tamko Na. 61/106 la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watu wenye Ulemavu linafasili kuwa, watu wenye ulemavu ni wale wote wenye matatizo ya muda mrefu ya viungo, akili, uelewa au hisia ambayo pamoja na vikwazo mbalimbali vya kintazamo na kimazingira yanazuia ushiriki wao kikamilifu na kwa ufanisi katika shughuli za kijamii kama watu wengine<sup>2</sup>. Naye Mahenge (2019) anafasili ulemavu kwamba ukihusishwa na mtu ni kushindwa au kuwa na vikwazo vinavyomzuia mtu kupata fursa sawasawa na watu wengine kutokana na changamoto za kimwili, kiakili au kijamii. Fasili hizi zimetusaidia katika mjadala wetu katika uandishi wa makala hii.

Ni vema kutaja idadi ya watu wenye ulemavu duniani, Afrika na Afrika Mashariki ili kujenga hoja kwa wasomaji umuhimu wa mada inayojadiliwa. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani, inakadiriwa kuwa zaidi ya watu bilioni 1 wana ulemavu duniani (WHO 2021). Kwa upande wa Afrika, inakadiriwa kuwa zaidi ya watu milioni 80 wana ulemavu (UN 2019) na kwa upande wa Afrika Mashariki inakadiriwa angalau watu milioni 18 wana ulemavu (EACPPD, 2012)<sup>3</sup> Hata hivyo, ni vigumu kupata takwimu sahihi ya watu wenye ulemavu katika nchi zinazoendelea kutokana na familia kuficha watu hao (MLYDS 2004, EACPPD 2012, Madafa 2016) na kutoelewa vizuri fasiri halisi ya ‘ulemavu’ (Gauluhanga 2018). Idadi ya walemavu inazidi kuongezeka siku hadi siku na hii inatokana na sababu mbalimbali zikiwemo ajali, matatizo ya jinzi za wazazi pamoja na magonjwa yasiyoambukiza. Kuwapo kwa watu wenye ulemavu katika jamii ndiko kumeibua methali husika zinazoakisi kundi hili, kwani fasihi kwa kiasi kikubwa hutokana na jamii husika (Mulokozi 2018).

Methali zilizokusanywa zinaonesha kuwa ulemavu hutokana na sababu tofauti tofauti na katika hatua mbalimbali za maisha ya binadamu. Kwa mfano, kuna ulemavu ambao mtu anazaliwa nao (taz. methali: ‘Cheka kilema uzae kilema’); upo ulemavu wa kupata ukubwani kutokana na sababu mbalimbali kama vile ajali au ugonjwa (taz. ‘Mpofuka ukongweni hapotewi na njia’, na ‘Mcheka kilema hafi hakijamfika’); ulemavu wa kutokana na kukosa umakini katika kufanya jambo fulani (‘Kilema cha kutafuta hakipewi pole’) na ulemavu kutokana na kudra ya Mungu (taz. ‘Mungu akikupa kilema hukupa na mwendo wake’). Methali za makala hii tumezitoa katika matini andishi ambazo ni Wamitila (2010) na King’ei & Ndalu (2009) na chache kutoka kwa Robert (2007) katika Mulokozi na mwenz. (2007) na Mrikaria (h.t). Pia

---

<sup>2</sup> <http://www.un.org/esa/socdev/enable/faqs.htm> Imesomwa tarehe 11 Machi 2014.

<sup>3</sup> EAC Policy on Persons With Disabilities (2012).

tulifanya usaili wa watu wenye ulemavu na wasio walemavu, ili kupata maoni yao kuhusiana na methali hizi.

Kutokana na data za methali tulizokusanya, ulemavu wa macho (upofu) na akili ndio unaotajwa mno<sup>4</sup>. Msisitizo wa umuhimu wa macho, mathalani, unajitokeza pia hata katika kisakale cha Kiswahili cha Nyoka kwenda kumuazima macho Jongoo na yeye kumpa miguu yake. Nyoka mpaka leo hajayarudisha macho hayo kwa jongoo. Nyoka hakuthamini tena umuhimu wa miguu aliyonayo, hivyo ameona ni vema atembe kwa tumbo lakini aone yanayojiri duniani! Dhana ya chongo kuonekana kuwa ni mfalme mbele ya ‘vipofu’ pia inadhihirisha umuhimu wa macho, kwani ufalme ni mojawapo ya vyeo vikubwa vya kiutawala. Ualbino na ukiziwi haujatajwa kabisa na ububu umetajwa mara chache sana. Labda huenda jamii ilichukulia kuwa, aina hizi za ulemavu si tatizo kubwa la kiafya la kuweza kumzuia mtu kufanya shughuli zake sawa na mtu mwingine yeyote ambaye hana ulemavu. Tunakiri pia kwamba inawezekana kuna aina nyingine za ulemavu ambazo hazijatajwa kabisa katika methali hizi. Kwa mujibu wa watafitiwa wetu, kujitokeza kwa methali chache kuhusu ulemavu wa ualbino kunaweza kutokana na sababu kwamba katika jamii nyingi za Kiafrika, watu wenye ulemavu wa ualbino walikuwa wakifichwa ndani ya nyumba na/au kuuawa (taz. Mahenge 2019). Unyanyapaa huo ulisababisha watu wenye ulemavu wa aina hii kutotajwa katika methali kama ilivyo kwa aina nyingine za ulemavu kama vile wa macho au miguu. Suala la kuua au kuwaangamiza walemavu linajitokeza pia, mathalani, katika utafiti wa Christensen (1963) na jambo hili limekuwepo duniani kote (Mahenge 2019). Utafiti wa Christensen unaozungumzia utani katika jamii ya Waluguru nchini Tanzania, unaelezea kwamba, hapo zamani katika “jamii ya Waluguru, watani walishiriki mambo mbalimbali ikiwemo kuua watoto. Watoto waliojulikana kama *kigego* walionekana kuwa ni hatari hivyo waliuawa. *Kigego* ilijumuisha mmojawapo wa watoto mapacha, ulemavu wa ualbino, watoto wa ajabu sana, au watoto waliozaliwa kwa kutanguliza matako.”

Nadharia tuliyotumia katika uchambuzi wa data ni Mwitiko wa Msomaji<sup>5</sup>. Nadharia hii ilipata mashiko mwishoni mwa miaka ya 1960 na mwanzoni mwa miaka ya 1970. Nadharia hii imechota baadhi ya hoja zake kutoka nadharia ya Hemenitiki (taz. Holub 1989, Thompson 1993). Miongoni mwa wananadharia hii ni Rosenblatt (1969), Wolfgang Iser (1978), na Stanley Fish (1978).

---

<sup>4</sup> Ingawa methali tunazorejelea katika makala hii zinawakilisha jamii ya Waswahili Afrika Mashariki, kwa upande wa Tanzania takwimu zinaonesha kwamba, ulemavu wenye idadi kubwa ya watu ni wa kuona ukifuatiwa na kutembea, kumbukumbu, kusikia, kujihudumia, kuwasiliana na ualbino (taz. <https://www.nbs.go.tz/index.php/en/census-surveys/health-statistics/disability-statistics/102-intergrated-labour-force-survey-2014-disability-statistics>)

<sup>5</sup> Ingawa methali ni kipera cha fasihi simulizi na hutumika sana katika mazungumzo ya kawaida nadharia hii imetumika kwa sababu data zilizotumika zimekusanywa kutoka katika matini andishi.

## METHALI ZA KISWAHILI ZIHUSUZO ULEMAVU

Katika nadharia hii, msomaji anapewa uwezo wa kufasiri na kutathmini matini anayoisoma na kuipa maana. Mathalani, Iser (1978) ana mawazo kuwa hakuna njia moja iliyo sahihi na toshelevu ya kufasiri matini ili kupata maana kamilifu. Wasomaji tofauti huwa na fasiri zao tofauti (katika Eagleton 1996, Wamitila 2002, Wafula & Njogu 2007). Nadharia hii inalenga katika matini na jinsi inavyosomwa na kufasiriwa na msomaji. Maana ya matini ya kifasiri haina kikomo na hupatikana katika zoezi la usomaji. Hivyo, wasomaji tofauti katika kipindi kimoja, msomaji mmoja katika vipindi tofauti na wasomaji tofauti katika vipindi tofauti wataielewa matini husika tofauti. Maana hutofautiana kutokana na nani anaisoma matini, wapi, lini, kwa matarajio gani na kwa madhumuni gani (Nixon 1985, Thompson 1993, Abrams 1999). Jukumu kubwa la msomaji ni kuisoma kazi kwa umakini na hatimaye kufasiri kazi hiyo kutokana na uwezo wake (Wafula & Njogu 2007), mazingira aliyomo na uelewa wake. Madhumuni ya makala hii ni kufafanua mitazamo inayotokana na methali za Kiswahili kuhusu ulemavu na watu wenye ulemavu. Kwa hivyo, kutokana na uelewa wetu wa methali hizi tunaona kuwa nadharia hii imefaa kuchambulia data zilizowasilishwa. Methali hizo kama tulivyosema awali tumezitoa katika matini andishi ambamo zimehifadhiwa.

### **Uchambuzi wa Mitazamo kuhusu Methali Husika**

Wasanii hutazama mambo kwa namna mbili: Kwanza, huutazama ulimwengu au mazingira yanayomzunguka binadamu kiyakinifu-kisayansi, yaani huuona ulimwengu kuwa ni kitu kinachobadilika kufuatana na mfumo wa kihistoria. Mtazamo wa pili ni wa kidhanifu ambao huuchukulia ulimwengu kama kitu kinachobadilika kulingana na matakwa ya Mungu (Msokile 1993). Mtazamo ni jinsi msanii au mtu anavyochukulia au kufikiria juu ya jambo fulani. Ni mawazo ya mtu kuhusu jambo fulani (Oriedo 2007). Mtazamo wa msanii hujigeza katika falsafa yake kuhusu masuala mbalimbali ya jamii (Madumulla 2009). Kwa kuwa fasili hii ya Madumulla imetaja falsafa hatuna budi kufasili dhana hiyo japo kwa ufupi. Falsafa ni wazo ambalo mtu anaamini lina ukweli fulani unaotawala maisha yake pamoja na maisha ya jamii (Msokile 1993). Aidha, falsafa ni mchujo wa welekeo wa mawazo muhimu yanayojitokeza kila mara katika kazi mbalimbali za msanii (Senkoro 2011). Hivyo, mtazamo ni namna mtu anavyolitazama jambo lililopo mbele yake, kulingana na msimamo wake wa kimaisha. Kwa maana hii, ni namna mtu anavyoliona jambo fulani. Methali kuhusu ulemavu na watu wenye ulemavu zimesheheni mitazamo ambayo ilionekana ni muhimu na jamii katika kuiielewa dhana ya ulemavu na kuijenga jamii husika kuhusiana na uga huo. Tulikusanya methali 50, baada ya kuzichunguza na kwa mujibu wa maoni ya watafitiwa wetu methali hizo zinabeba mitazamo ifuatavyo:

### **Ulemavu Hauchekwi kwani Waweza Kumfika Mtu yeyote**

Kuwapo kwa methali za Kiswahili ambazo zinazungumzia ‘kumcheka mlemavu’ kunadhihirisha kuwepo kwa kitendo hiki katika jamii. Methali kama kazi ya fasihi mara nyingi huakisi jamii. Mtu mwenye ulemavu kuonekana kama kichekesho huweza kumfanya kujiona mnyonge. Hivyo methali hizi zinakemea tabia hii kwani kumcheka mtu mwenye ulemavu si jambo jema hata kidogo “kunamuathiri kisaikolojia na hivyo kujiona anakosa heshima, kujiamini na ulinzi. Aidha, mlemavu hujiona hana thamani, faida, manufaa, mbaya na mzigo kwa jamii” (Reeve 2006 katika Olaiya 2013). Methali hizi, mbali na kukemea kuwacheka walemavu, kwa upande mwingine zinawatia moyo watu wenye ulemavu na familia husika. Methali husika zinabainisha kuwa:

1. ‘Achekaye kilema hata kwao kipo’ (Wamitila 2010:Na.10<sup>6</sup>, King’ei & Ndalul 2009:8)<sup>7</sup>.
2. ‘Cheka kilema uzae kilema’ (Wamitila 2010:344, King’ei & Ndalul 2009:311).
3. ‘Cheka uchafu (na uvivu) usicheke kilema’ (Wamitila 2010:345, King’ei & Ndalul 2009:312).
4. ‘Mcheka kilema hafi hakijamfika’ (Wamitila 2010:1063, King’ei & Ndalul 2009:1184).

Methali hizi zinalenga kubadili tabia za wanajamii kwamba hawapaswi kuwacheka walemavu. Mathalani, baadhi ya familia hapo zamani (na nyingine hadi hivi leo) zilificha na zinaendelea kuficha watoto au watu wenye ulemavu (Mahenge 2013b) na wengine huwaua watoto wao walemavu kwa kuogopa kupata aibu ya kuchekwa na watu (Dandi 2015). Tabia ya wazazi kuficha watoto wao wenye ulemavu zinawafanya watoto hao kukosa huduma muhimu na stahiki za jamii (MLYDS 2004)<sup>8</sup>. Methali hizi zinanasihi kuwa ulemavu hauna mwenyewe, na mtu yeyote unaweza kumfika ama kwa kuzaliwa nao, au kwa kuupata ukubwani, kwani kabla hujafa hujaumbika. Aidha, methali zinashauri kuwa kama unajisikia kucheka ni vema kucheka uchafu na uvivu, lakini si ulemavu. Kwa upande mwingine, methali hizi zinaelimisha kuhusu masuala mengine, ikiwemo kukemea uchafu na uvivu katika jamii kwani huweza kusababisha maradhi na njaa. Hivyo, kwa kupitia methali hizi dhamira mbalimbali pia zinaibuliwa kama vile umuhimu wa usafi wa mazingira, ufanyaji kazi katika jamii, uzazi na kifo.

---

<sup>6</sup> Namba hii inawakilisha namba ya methali katika kitabu husika, siyo namba ya ukurasa katika kitabu hicho. Hata hivyo, kwa methali tulizozipata kutoka kwa Mrikaria tumetumia namba ya ukurasa kwa sababu hakuweka namba kwenye methali.

<sup>7</sup> Kama tulivyoeleza hapo awali, methali hizi tumezikusanya kutoka katika matini andishi.

<sup>8</sup> Ministry of Labour, Youth Development and Sports.

## METHALI ZA KISWAHILI ZIHUSUZO ULEMAVU

### **Mlemavu Hastahili Kushiriki au Kupata baadhi ya vitu**

Katika nchi nyingi zinazoendelea umaskini unapunguza uwezekano wa watu wenye ulemavu kupata huduma za kijamii kama vile elimu, afya na haki nyingine za kimsingi ikilinganishwa na watu ambao hawana ulemavu (Rutachwamagyo 2000). Hivyo, programu nyingi za maendeleo hazizingatii mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu kinyume na makubaliano ya kimataifa yanayosisitiza uzingatiaji huo kwa ajili ya maendeleo endelevu (Mushumbusi 2016). Mbali na umasikini na usaguzi, unyanyapaa kutoka kwa jamii unazidi kuongeza machungu ya watu wenye ulemavu na kukosa au kutoshirikishwa katika baadhi ya mambo. Methali zifuatazo zinadhahirisha jambo hili japo kwa uchache:

5. ‘Mcheza hawi kiwete, ngoma yataka matao’ (Wamitila 2010:1069, King’ei & Ndalu 2009:1193).
6. ‘Kipofu ha-hitaji miwani’ (Mrikaria h.t:152).
7. ‘Kumshauri mtu mpumbavu ni kama kumpa kipofu miwani ya kuonea ambayo haihitaji’ (Mrikaria h.t:161).
8. ‘Kumwashia taa pofu ni kuharibu mafuta’ (Wamitila 2010:838, Mrikaria h.t:161).

Methali Na. 5, mbali ya kuonesha utamaduni wa Mwafrika hususani uchezaji wa ngoma, linalosisitizwa ni hali ya mchezaji, kwamba hapaswi kuwa kiwete. Hii itamfanya kutocheza kiukamilifu na kwa ufanisi kama ambavyo mtu ambaye si mlemavu hucheza. Methali kama hizi si tu zinawatenga walemavu kushiriki katika michezo na fani mbalimbali bali pia zinaua vipaji vyao na hata kusababisha ‘Njozi zao kupotea’ (taz. Mung’ong’o 1980). Aidha methali hii inapingana na sheria za kimataifa zinazosisitiza kwamba watu wenye ulemavu wana haki ya kushiriki shughuli za kiutamaduni, michezo na burudani mbalimbali (taz. Kifungu Na. 30 UN-CRPD 2006). Hata hivyo katika uhalisia, watu wenye ulemavu wa viungo wamekuwa wakionekana kushiriki katika sanaa ikiwemo uchezaji wa muziki (taz. T.O.T Band wimbo ‘Mtaji wa Masikini’, Rose Muhando wimbo ‘Nibebe’, Miriam Thomas Chiwa wimbo ‘Unitambulisho Yesu’) na michezo mingine mbalimbali kama vile mashindano ya watu wenye ulemavu duniani maarufu kama *Paralympics* yaliyoanza mwaka 1960 huko Italia na mpaka sasa walemavu kutoka katika nchi mbalimbali wamekuwa wakishiriki na kufanya vizuri tu na kuziletea nchi zao medali mbalimbali.

Jambo jingine ambalo mtu mwenye ulemavu, hususani asiyeona, hapaswi kuwa nalo ni miwani. Miwani ni kifaa kinachoweza kuvaliwa kama pambo, kuinga miali mikali ya jua, kuimarisha uoni ama kusomea. Wakati methali Na. 6 haielezi miwani ambayo mlemavu asiyeona hastahili kuwa nayo, methali Na. 7 inaeleza kuwa ni miwani inayosaidia kuona. Methali hii, mbali na dhahaka na kejeli, pia inatumia tashibiha ambapo ‘ushauri’ unalinganishwa na ‘miwani

ya kuonea’, na ‘mpumbavu’ analinganishwa na ‘kipofu’. Methali inaona mpumbavu hastahili kupata ushauri kama ambavyo ‘kipofu’ hastahili kuwa na ‘miwani’. Mbali na kunyimwa miwani, ‘kipofu’ katika methali Na. 8, hastahili kuwashwa taa kwani ni uharibifu tu wa mafuta (au umeme). Methali hizi zinaonesha kuwa, “Tatizo kubwa ambalo mlemavu anakumbana nalo si tu ulemavu wenyewe bali usaguzi na mitazamo hasi kutoka kwa jamii kuhusiana na ulemavu na vikwazo vya kimazingira ambavyo vinadunisha uwezo wake” (Teferra 1994:43). Methali zinaonesha kwamba “watu wenye ulemavu wanakumbana na vikwazo katika jamii katika kushiriki mambo mbalimbali kama mwanajamii na hivyo haki zao kukiukwa duniani kote” (UNCRPD 2006:2)<sup>9</sup>

Kwa mujibu wa watoataarifa wetu methali hizi ziliwajenga na kuendelea kuwajenga wanajamii kuamini kuwa mlemavu hapaswi kuendelezwa au kushirikishwa katika masuala mbalimbali kama vile michezo na burudani, elimu, ajira, na uwezeshwaji kiuchumi. Haki za walemavu zinapinga kubaguliwa kwa walemavu kwa ajili ya upungufu walionao. Masuala ya kumwona mlemavu kuwa hastahili jambo fulani yamekuwa na athari kwa maendeleo yao na hata kwa jamii inayowazunguka. Athari hizo zinaonekana katika sekta mbalimbali kama vile ujenzi wa majengo yenye kukosa miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu wa viungo ambao wanatumia vitimwendo kutembelea, uhaba wa shule za watu wenye mahitaji maalumu, na kukosa kuajiriwa. Aidha, ukosefu wa rasilimali na fursa za kiuchumi na mitazamo kama hii inafanya baadhi ya wazazi au walezi kuona kwamba hakuna sababu ya kumpeleka mtoto mwenye ulemavu shule. Matokeo yake kufanya idadi ya watoto wenye ulemavu wanaosajiliwa kwenye shule kuwa ndogo ukilinganisha na watu ambao hawana ulemavu ambao wanaaminiwa ndio wanachangia katika maendeleo ya kiuchumi ya nchi husika (Deku 2002, Kristensen & Omagor-Loican & Onen 2003). Hivyo, wanakosa fursa nyingi za kiuchumi na kijamii kama vile elimu ambazo ni muhimu sana kwao kwa ustawi wao maishani (Stone-MacDonald 2012). Kwa mfano, nchini Tanzania ingawa kuna shule za watu wenye ulemavu lakini hazitoshi kukidhi mahitaji yao. Mbali ya kuwapo kwa vyama mbalimbali vya watu wenye ulemavu, asasi ambazo zinashughulikia maslahi yao zimechelewa kuanzishwa. Mathalani, nchini Tanzania ni kuanzia miaka ya 2000 ndipo watu wenye ulemavu wameanza kupata uwakilishi katika vyombo vya kisheria kama vile bungeni, na Wizara ambayo, pamoja na mambo mengine, inashughulikia watu wenye ulemavu imeundwa kwa mara ya kwanza mwaka 2015<sup>10</sup>. Hali hii inaonesha kuwa kwa muda mrefu kilio na malalamiko yao yalikuwa hayasikilizwi ipasavyo au kufikishwa katika ngazi za juu za kiutawala. Aidha, ni zaidi ya nusu karne sasa tangu Tanzania ipate uhuru ambapo ni Aprili 11 2016 Ofisi ya Taifa ya Takwimu wakishirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu walizindua kanzidata (*database*)

---

<sup>9</sup> United Nations Convention on the Rights of Persons with Disabilities (2006).

<sup>10</sup> Wizara ya Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu.

## METHALI ZA KISWAHILI ZIHUSUZO ULEMAVU

ambayo ina takwimu muhimu kuhusu taarifa za watu wenye ulemavu nchini. Kanzidata hii itasaidia upatikanaji wa taarifa sahihi za watu wenye ulemavu na hatimaye kupanga mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa ajili ya maendeleo endelevu (Mushumbusi 2016).

Kinachobainika katika methali zilizorejelewa hapa ni kwamba, watu wengi *walikuwa* hawajatambua uwezo wa watu wenye ulemavu kama wanaweza kuendelezwa kwa ukamilifu (Teklu 2010:97 msisitizo wetu) au kushirikishwa katika kupata fursa na mahitaji mbalimbali ya kijamii. Badala yake jamii na kwa kupitia methali imejaa usaguzi kwa watu wenye ulemavu ambao unarudisha nyuma maendeleo yao. Kwa kurejelea Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji tunaona hapa kwamba kusoma si suala la kutafuta maana ya matini *tu*, bali ni mchakato wa uzoefu wa kujua matini inakufanyia nini (Eagleton 1996:74 msisitizo ni wetu). Hivyo, tunaona kuwa methali kama hizi zilimrudisha na zinamrudisha nyuma mtu mwenye ulemavu katika ustawi wake maishani.

### **Mlemavu wa Akili Asikilizwe kwa Makini**

Wahenga wanatilia mashaka uyakini wa maneno ya mtu mwenye ulemavu wa akili (mwendawazimu) taz. Na. 9 na kuona kuwa hayana maana taz. Na. 10 lakini wakati huohuo wanatambua kuwa yanaweza kusikilizwa lakini kwa umakini mkubwa taz. Na. 11. Tazama mifano ifuatayo:

9. ‘Ajabu ya kusikia uyakini kutokana na mwendawazimu’ (Mrikaria h.t:19).
10. ‘Maneno ya mwendawazimu hayana maana lakini ni maneno’/ ‘Maneno ya mwenda uwazimu ni maneno’ (Wamitila 2010:1006, King’ei & Ndalu 2009:1112).
11. ‘Akisema mwendawazimu, msikiaji awe na akili’ (Wamitila 2010:70, King’ei & Ndalu 2009:57).

Methali hizi zinasisitiza haki ya kusikilizwa kwa kila binadamu bila kujali kama ni mwendawazimu au kama anachokisema kina ukweli. Wahusika ambao ni wendawazimu, vichaa au machizi wamekuwa wakitumiwa katika baadhi ya kazi za fasihi kuwasilisha jumbe muhimu katika kazi husika. Mathalani, Penina Mhando katika tamthiliya yake ya *Nguzo Mama* (1982) anamtumia mhusika Chizi<sup>11</sup> ili kuwasilishia mambo mazito/muhimu ya kuwahamasisha wanawake waungane kwa pamoja ili waweze kuisimamisha nguzo yao kama wao kwani uwezo wanao, jambo la msingi ni kufanya kazi kwa kushirikiana. Wahusika wendawazimu huweza kutumika pia katika kazi za fasihi ili kukwepa uhibitaji. Lengo mojawapo la matumizi ya

---

<sup>11</sup> Chizi ni mtu ambaye ana matatizo ya afya ya akili (BAKITA 2017:138) na mwendawazimu ni mtu ambaye akili zake zimevurugika na hivyo si timamu na aghalabu huweza kuwa anazungumza mwenyewe au kufanya matendo yasiyotarajiwa (BAKITA 2017:789).



wahusika ambao ni machizi katika kazi ya fasihi ni kuonesha ukweli fulani wa mambo, ndivyo hivyo methali hizi zinaonesha ukweli fulani kuhusiana na mwendawazimu. Msikiaji awe na akili ya kutafakari kwa kina kile anachoambiwa na mwendawazimu.

### **Bora Ulemavu kuliko Kifo**

Suala la kifo linajitokeza pia katika methali mbalimbali (taz. pia Na. 4). Methali zinaonesha kuwa kama ingelikuwa mtu anachagua kati ya ulemavu na kifo, basi aheri ya ulemavu kuliko kifo! (taz. Na. 12). Mathalani, methali zinabainisha kuwa ingawa ulemavu si jambo la kulitaka na hakuna mtu anayependa kupoteza kiungo chake, lakini inaelezwa kuwa ni afadhali ‘kulemaa’ au kufa macho kuliko kufa kabisa kama methali zifuatazo zinavyodhihirisha:

12. ‘Bora kilema kuliko mfu’ (Wamitila 2010:305, King’ei & Ndalal 2009:267).
13. ‘Heri kufa macho kuliko kufa moyo’ (King’ei & Ndalal 2009:548).

Methali hizi si tu zinaonesha kuwa “katika falsafa ya jamii za Kiafrika kifo ni kitu ambacho kinamchanganya sana binadamu” (Mbiti 2011:44-5) bali pia zinabainisha kwamba kama kifo kingekuwa hakipo basi ulemavu si kitu kizuri kuwa nacho. Kwa namna hii zinawafanya walemavu wajione kama watu dhaifu mbele ya jamii. Hii ni kutokana na ukweli kwamba “kwa Waafrika, methali zinachukuliwa kama urithi wa kiutamaduni unaozingatiwa sana kutokana na imani kwamba zimefumbata falsafa, busara na maarifa ya jamii” (Balogun 2006:87).

### **Mwanamke Mzuri Lazima awe na Kilema**

Usawiri wa mwanamke katika kazi mbalimbali za fasihi umejadiliwa sana. Matokeo ni kwamba katika kazi hizo mwanamke anachorwa katika sura mbili; hasi na chanya. Picha inayoonekana zaidi ni ile ya uhasi ambapo mwanamke anaonekana kama kiumbe dhaifu (taz. Momanyi 2001, Omari 2008). Usawiri huo unatokana na mambo kadhaa kama vile waandishi wengi wa kazi za fasihi kuwa wanaume (Mbughuni 1982) na kushamiri kwa mfumo dume ambapo mwanamke anaonekana duni akilinganishwa na mwanaume (Momanyi 2001, Khamis 2019). Waswahili wanasema katika msafara wa mamba (walemavu) na kenge (wanawake) nao wamo, yaani katika methali zihusuzo watu wenye ulemavu, mwanamke pia anasawiriwa. Naye anachorwa katika sura mbili; chanya (mzazi, mlezi na mwaminifu) na hasi (ana kasoro/kilema cha kitabia). Hakuna methali, kutokana na data zetu, kuhusiana na ulemavu ambayo inamtaja mwanaume. Mfano wa methali hiyo kuhusu mwanamke na ukilema/kasoro ni:

14. ‘Mwanamke mzuri hakosi kilema’ (Wamitila 2010:1420, King’ei & Ndalal 2009:1617).

## METHALI ZA KISWAHILI ZIHUSUZO ULEMAVU

Kilema ni kasoro iliyoko kwenye kiungo au viungo vya mwili au mtu mwenye upungufu wa kiungo kama vile kiwete. Katika methali hii kinachorejelewa hasa ni kasoro katika tabia kama vile uvivu, wizi, uchafu, na uongo. Ingawa kwa maana pana methali hii inaweza kutumika kuwakilisha jinsia zote (mwanamke na mwanaume) lakini hapa mfano umetolewa kupitia kwa mwanamke. Methali inamaanisha kuwa mwanamke ndiye mwenye kasoro, si mwanaume. Swali ni Je, wanaume wazuri hawana vilema (kasoro?). Kwa namna fulani, jamii imeendelea kumdunisha mwanamke kwa methali zinazohusianishwa na ulemavu. Kwa mfano, kuna msemu<sup>12</sup> mwingine ambao unahusisha mwanamke na mlemavu wa macho usemao ‘Wanawake mwalimu wao ni kipofu’. Kwa kupitia methali na hata misemo (ingawa si lengo la makala yetu kuchambua misemo) hii ni wazi kuwa wanawake na watu wenye ulemavu wanaathirika kisaikolojia. Aidha, kama ilivyo kwa methali ambazo tumeona hapo mwanzo, methali Na.14 pia inashadidia usaguzi wa kijinsia na unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu katika jamii ya Waswahili.

### **Ulemavu hususani kwa Mwanamke una Manufaa yake**

Jamii ya Waswahili, kupitia baadhi ya methali, inaona kwamba ulemavu una manufaa fulani kijinsia, hususani akiwa nao mwanamke. Mathalani, manufaa ya ulemavu wa macho kwa mwanamke ni kama ifuatayo:

15. ‘Mke kipofu huwa mwaminifu’ (Wamitila 2010:1166).
16. ‘Mke kipofu huangaza nyumba’ (King’ei & Ndalal 2009:1304).

Methali hizi zinamwangazia mwanamke mlemavu wa macho katika ndoa. Dhana ya uaminifu ni pana lakini inatumika sana pia katika uga wa mapenzi. Kwa mfano, kuna msemu kwamba ‘kuwa na mpenzi mmoja, tumia kondomu au kuwa mwaminifu’. Methali hii inaonekana kwa namna fulani kuwahimiza wanaume wawaoe wanawake wenye ulemavu wa macho kwani wana manufaa, si wakware si wadanganyifu; ni waaminifu. Hivyo ulemavu wa macho una manufaa yake na hasa akiwa nao mwanamke (mke). Ingawa hatujui methali hii iliundwa na jinsia gani lakini inampaka mwanamke mafuta kwa mgongo wa chupa. Inaonekana kumsifia mwanamke ‘kipofu’ kwa uaminifu lakini ‘ukweli’ unaomaanishwa hapa ni kwamba kitabia wanawake wengine wote ambao si ‘vipofu’ si waaminifu; ni wakware na wadanganyifu katika mambo mbalimbali. Lakini je wanaume hawana tabia hiyo? Kwa nini mifano kama hii ipitie kwa mwanamke? Nini athari za methali kama hii kwa malezi ya watoto na vijana wa jinsia zote?

Maoni yetu ni kwamba kumwona mwanamke kama ni kiumbe chenye kasoro au si mwanamifu kama hana upofu kupitia methali zihusuzo walemavu si tu kunamdunisha mwanamke bali na watu wenye ulemavu pia. Kwa upande mwingine “Methali hii inasisitiza kuwa binadamu

---

<sup>12</sup> Makala yetu inahusu methali lakini tumeona kwamba msemu huu ni muhimu kuurejelea ili kuimarisha mjadala wetu.

hanyimwi yote; anaweza kuwa na upungufu fulani lakini akawa na mambo mengine mazuri” (taz. Wamitila 2010:169); ‘Aso hili ana lile’.

### **Baba Huweza Kumkana Mtoto mwenye Ulemavu**

Kuzaa mtoto mlemavu si jambo ambalo wazazi wanalitarajia na hivyo kusababisha wakati mwingine baba kuweza kumkana mtoto husika. Methali ifuatayo inathibitisha jambo hili:

17. ‘Mama hawezi kumkana mtoto hata akiwa na kilema’ (Wamitila 2010:985).

Tabia ya kumkana mtoto mwenye ulemavu inatokea duniani kote (Van Campen & Van Santvoort 2013). Methali hii inadokeza kuwa kwa kuwa mwanamke ndiye anabeba mimba ni dhahiri kuwa mwana amzaaye ni wa kwake. Lakini kwa mwanaume mtazamo ni kwamba inawezekana kabisa mtoto akawa si wa kwake bali ni wa baba mwingine. Jambo ambalo pia linaweza kuwa na ukweli kwa kiasi fulani kutokana na tafiti mbalimbali zihusuzo kupima vinasaba (taz. John 2016). Suala hili linachangiwa kwa kiasi fulani kwa mwanamke kuonekana kuwa si mwaminifu katika mahusiano ya kindoa (taz. Na. 15). Methali hii pia inaonesha tabia iliyopo katika jamii ya baadhi ya wazazi wa kiume kuwakataa watoto wao walemavu (Mahenge 2013a). Baadhi ya wanaume huweza kuzikimbia familia zao pindi wake zao wanapojifungua watoto wenye ulemavu, ikiwemo albino, kwa imani kuwa ni mkosi (taz. Milton 2017). Methali hii inaweza kuwakilisha kilio cha wanawake kuhusu jambo hili na / au maoni ya jamii nzima kuhusu tabia iliyopo katika jamii ya baadhi ya akina baba (wanaume) kuwakataa watoto wenye ulemavu. Kuwepo kwa teknolojia ya kupima vinasaba (DNA) katika jamii ya sasa kunaweza kupunguza tatizo hili la kukataa watoto hawa. Kumkana mtoto mwenye ulemavu si tu kunaongeza unyanyapaa dhidi yake na kumfanya mtoto kupata malezi ya upande wa mama tu bali pia mtoto huyo anaonekana kama ni aibu, “kiumbe asiye hitajika na mzigo kwa familia katika malezi yake” (Olaiya 2013:144) na hata kumsababishia unyonge. Methali hii pia inaonesha nafasi ya mama katika mapenzi na malezi ya mtoto.

### **Mungu ni Muweza wa yote**

Katika jamii za Kiafrika ulemavu unaweza kutazamwa kuwa unatokana na imani za kiutamaduni, kidini (Devlieger 1999, MLYDS 2004), laana, adhabu ya miungu kwa wazazi waliotenda dhambi, kurithi, uchawi (taz. Berghs & Dos Santos-Zingale 2011, Olaiya 2013), sababu za kimatibabu na kiafya au mpango wa Mungu (Stone-MacDonald 2012). Katika methali ambazo tumekusanya kuhusu ulemavu nafasi ya Mungu ndiyo inajitokeza zaidi:

18. ‘Chongo kwa Mnyamwezi kwa Mswahili rehema ya Mungu’ (Robert 2007:217).

19. ‘Mungu akikupa kilema hukupa na mwendo wake’ (Wamitila 2010:1367, King’ei & Ndalu

## METHALI ZA KISWAHILI ZIHUSUZO ULEMAVU

2009:1553, Mrikaria h.t:217).

Kuhusiana na Wanyamwezi, mbali na methali Na. 18 pia kuna msemu mwingine wa Kiswahili usemao ‘Mzigo mzito mpe Mnyamwezi’. Historia inaonesha, katika karne ya 19 wakati wa utawala wa Waarabu, Wanyamwezi nchini Tanzania walikuwa ni miongoni mwa makabila ambayo yalishiriki kubeba mizigo kama vile pembe za ndovu na bidhaa nyingine katika misafara ya biashara. Hali hii ilizua utani miongoni mwa jamii zilizokuwa pwani kama vile Wazaramo. Mathalani, Wazaramo waliamini mizigo mizito ambayo wengine iliwashinda kubeba, basi Mnyamwezi alikuwa na uwezo wa kubeba kutokana na kwamba alikuwa na nguvu. Methali Na. 18, kwa kiasi fulani inaonekana kuibuka katika mazingira haya ya utani. Methali kwa mapana yake inaonesha Mungu ndiye humpa mtu ulemavu na ndiye mtawala wa maisha ya binadamu, kwa uzima na kwa ugonjwa. Hivyo basi ulemavu ni rehema na mapenzi ya Mungu; na pindi Mungu anapokupa ulemavu basi anakuwa ameshakupangia namna utakavyoweza kuendesha maisha (methali Na. 19). Methali hii kwa kumrejelea Mbiti (1975, 2011:2) inaonesha kuwa mifumo ya kifalsafa ya Kiafrika huweza kubainika kupitia “umbo la dini, methali, fasihi simulizi na maadili.” Methali inatia moyo na kumjenga mlemavu kiakili kwamba hata kama akichekwa, akikimbiwa na mzazi na kadhalika, Mungu yuko naye.

### **Ulemavu si Kikwazo kwa Apendaye**

Eneo lingine ambalo methali hizi zihusuzo watu wenye ulemavu linatutazamisha ni kuhusu mapenzi. Hata hivyo, hatukupata methali za kutosha kuhusiana na suala hili. Methali ifuatayo inazungumzia suala hilo la ulemavu na mapenzi:

20. ‘Akipenda chongo huita (huona) kengeza’ (Wamitila 2010:68).

Hata hivyo, methali kuhusiana na kupenda na ulemavu hazitaji aina mbalimbali ya walemavu badala yake inataja chongo (mtu ambaye ana jicho moja lisiloona) ingawa maana inayowakilishwa inaweza kuwa pana zaidi. Kwamba, matatizo katika kiungo cha mwili si tatizo kwa mwenye mapenzi ya kweli kwani ‘mwenye mapenzi haoni ingawa macho anayo’. Mwenye mapenzi haoni dosari. Jambo hili tunaweza kuliona hata katika jamii mbalimbali za Kiafrika kuwa, watu wenye ulemavu wanaolewa au kuoa watu wasio na ulemavu.

### **Mjadala zaidi**

Kupitia methali kuhusu ulemavu, jamii imekuwa ikijenga mitazamo, mafunzo na athari mbalimbali. Kuna mitazamo inayojenga na inayobomoa jamii na kuendelea kumuacha mlemavu nyuma kimaendeleo na kifursa. Methali zina thamani na nguvu kama nyenzo katika malezi ya watoto na kufundishia shuleni masuala mbalimbali ya binadamu kama vile lugha, dini na uzoefu wa jamii. Hii inatokana na ukweli kwamba, methali zina mafunzo yenye busara (Mieder 1997,

Momoh 2000). Hivyo, methali zenye mitazamo hasi kuhusu jambo fulani kama vile udunishaji na usaguzi kwa walemavu zinaimarisha unyanyapaa katika jamii. Jambo ambalo si jema kwa ustawi na haki sawa kwa wanajamii. Kwa kuwa methali hizi zimekuwapo katika jamii tangu kale na jamii inaendelea kujifunza kutoka kwazo, mitazamo hiyo hasi haina budi kubadilika. Mathalani, methali Na. 5-8 katika mukatdha mpana zinaweza kuendelea kusababisha mtu mwenye ulemavu kutoshirikishwa kwa ukamilifu katika shughuli mbalimbali za jamii, kunyanyapaliwa, kukosa fursa mbalimbali au baadhi ya huduma katika jamii kama vile elimu, afya, michezo na kadhalika. Baadhi ya methali zinapingana na sera na sheria mbalimbali za kitaifa na kimataifa kuhusu watu wenye ulemavu kama vile UNCRPD (2006), MLYDS (2004)<sup>13</sup> na EACPPWD (2012) ambazo zinasisitiza utu, ulinzi na usawa wa binadamu na zinapinga kumtenga au kumbagua mtu mwenye ulemavu katika masuala mbalimbali kama vile afya, ajira, elimu, kupata habari na kadhalika.

Kwa kupitia methali hizi tunaweza pia kupata falsafa ya Kiafrika. “Falsafa ya Kiafrika ni uelewa, mawazo, mantiki na mtazamo ya jinsi Waafrika wanavyofikiri, tenda au kuzungumza katika miktadha mbalimbali ya maisha” (Mbiti 2011:2). Miongoni mwa vyanzo vya falsafa ya Kiafrika ni mila simulizi kama vile methali na kazi andishi za Afrika (Oruka 1991, Oladipo 2002, Azenabor 2009, Mbiti 2011). Methali zinaaminiwa kuwa zimetokana na kutungwa na wazee wa jamii ingawa kwa sasa wanasiasa na vijana wana nafasi kubwa katika utunzi wake (taz. Kipacha 2014, Omari 2016). Miongoni mwa mambo yanayohusiana na falsafa ya Kiafrika yaliyojitokeza katika methali hizi ni suala la hofu ya kifo (Na. 12 na 13), umuhimu wa uzazi (kuwa na watoto) katika familia kwamba iwapo utamcheka mlemavu inawezekana katika uzao wako nawe ukazaa mtoto mlemavu (Na. 2) na ukuu wa Mungu katika maisha ya binadamu (Na. 18 na 19).

Jumbe zinazopatikana katika methali zinazohusu walemavu zinaweza kutumika kurejelea mafunzo na muktadha mpana na si tu katika dunia ya walemavu, kwa mfano:

21. ‘Ukila na kipofu usimguse mkono’ (Wamitila 2010:276).
22. ‘Ukienda kwa mwenye chongo fumba/vunja lako jicho’ (Wamitila 2010:1871, King’ei & Ndalu 2009:2160).
23. ‘Bubu hasemi lakini ipo siku atasema’ (Wamitila 2010:313, King’ei & Ndalu 2009:276).
24. ‘Haraka haraka ilimfanya mbwa azae watoto vipofu’ (Mrikaria h.t:121).

Methali husisitiza kufanya mambo kwa uangalifu, utaratibu (Na. 21), umakini (Na. 24) na kujifunza na kuishi kama watu wa jamii au kada fulani wanavyoishi (Na. 22). Aidha, inaelezwa kwamba mnyonge au anayeteseka ipo siku atadai haki yake (Na. 23). Methali kuhusu ulemavu

---

<sup>13</sup> National Policy on Disability (2004).

## METHALI ZA KISWAHILI ZIHUSUZO ULEMAVU

zinaangazia dhamira za mapenzi, haki, kifo, uzazi, tabia njema, dini, umaskini, umuhimu wa usafi wa mazingira na ufanyaji kazi. Methali hizi kama zilivyo methali nyingi za Kiswahili, zinafundisha, zinatia au kuvunja moyo, zinanasihi, zinaonya, zinahimiza mema au kukataza mabaya. Aidha, kwa mtazamo mpana, methali zinazotaja ulemavu huweza kurejelea mambo nje ya ulemavu. Kwa mfano, methali ‘Ukila na kipofu usimshike mkono’ ina maana pana zaidi kuwa, unapotenda jambo ulitende kwa umakini ili usiharibu mambo mengine.

### **Hitimisho**

Makala hii ililenga kuchunguza mitazamo ya methali za Kiswahili zihusuzo ulemavu na athari zake katika jamii. Kupitia methali tulizozichunguza tumeona kwamba methali hizo zinawasilisha mitazamo mbalimbali ya jamii. Mitazamo hiyo ni ulemavu hauchekwi kwani waweza kumfika mtu yeyote, mtu mwenye ulemavu hastahili kushiriki au kupata baadhi ya vitu, na mlemavu wa akili asikilizwe kwa makini. Mitazamo mingine ni bora ulemavu kuliko kifo, mwanamke mzuri lazima awe na kilema fulani, ulemavu hususani kwa mwanamke una manufaa fulani, baba huweza kumkana mtoto mwenye ulemavu, Mungu ni muweza wa yote na ulemavu si kikwazo kwa apendaye. Mitazamo hii ina athari katika jamii kwa mtu mwenye ulemavu na kwa jamii husika; athari hizo ni hasi na chanya. Imebainika kwamba baadhi ya methali huweza kumwathiri mtu mwenye ulemavu kisaikolojia, kumfanya kuwa mnyonge, dhaifu na kumsababishia akose haki na fursa fulani. Kwa kuwa methali hizi ni sehemu ya jamii yetu jamii inaweza kuzidi kuendeleza baadhi ya mambo kama vile kutompa haki mtu mwenye ulemavu (kama methali Na. 5-8 zinavyosisitiza). Athari nyingine ni kwamba methali hizi zinaendeleza usaguzi wa kijinsia kwa kumwona mwanamke kama ni kiumbe chenye kasoro fulani wakati mwanaume anapewa uhuru wa hata kumkana mtoto wake mwenye ulemavu. Suala hili si zuri kwa ustawi wa jamii. Methali hizi zina athari chanya chache sana ukilinganisha na hasi. Miongoni mwake ni kumtia moyo mtu mwenye ulemavu na hata jamii kuhusu nafasi ya Mungu katika maisha ya ulemavu.

Methali hizi zinafundisha, zinaonya, zinanasihi, zinarekebisha na hata kukatisha tamaa. Kwa kuzichanganua methali hizi imedhihirika kuwa, walemavu ni kundi ambalo lina changamoto za unyanyapaa na kutopewa fursa. Muhimu hapa ni kujenga jamii mpya ambayo haina unyanyapaa na ubaguzi kwa watu wenye ulemavu kwa mfano kwa kutoendelea kutumia methali zenye mtazamo hasi, kutozifundisha kwa watoto na kutunga methali mpya ambazo ni rafiki na zenye mtazamo chanya.

### **Marejeleo**

Abrams, Meyer H. 1999. *A Glossary of Literary Terms* (7<sup>th</sup> ed.). Boston: Heinle & Heinle.

SHANI OMARI MCHEPANGE & ELIZABETH GODWIN MAHENGE

- Azenabor, Godwin. 2009. Odera Oruka's Philosophic Sagacity: Problems and Challenges of Conversation Method in African Philosophy. *Thought and Practice: A Journal of Philosophical Association of Kenya* 1,1: 69-86.
- BAKITA, 2017. *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (Toleo la Pili). Nairobi: Longhorn Publishers Limited.
- Berghs, Maria & Myriam Dos Santos-Zingale. 2011. A Comparative Analysis: Everyday Experiences of Disability in Sierra Leone. *Africa Today* 58,2: 19-40.
- Balogun, Oladele A. 2006. A Jurisprudential Analysis of Yoruba Proverbs. *The Cambrian law Review* 37: 86-97.
- Christensen, James B. 1963. Utani: Joking, Sexual License and Social Obligations among the Luguru. *American Anthropologist*, 65,6: 1314-1327.
- Dandi, Tuma. P. 2015. Hujafa Hujambika. *Fanaka* 1: 21.
- Devlieger, Patrick J. 1999. Frames of Reference in African Proverbs on Disability. *International Journal of Disability, Development and Education* 46,4: 439-451.
- Deku, Prosper. 2002. Effects of Training in Community-Based Rehabilitation on Attitudinal Change of People toward People with Disabilities. *IFE Psychologia* 10,2: 175-184.
- Eagleton, Terry. 1996. *Literary Theory: An Introduction* (2<sup>nd</sup> ed.). Minnesota: The University of Minnesota Press.
- Gauluhanga, Christina. 2018. Takwimu za Walemavu Ziimarishwe. *Mtanzania*. 26 Juni 2018.
- Holub, Robert C. 1989. American Confrontations with Reception Theory. *Monatshefte* 81,2: 213-225.
- Iser, Wolfgang. 1978. *The Act of Reading: A Theory of Aesthetic Response*. London: Johns Hopkins University Press.
- John, Devotha. 2016. Are you unknowingly raising another man's child? *The CitizenTz* May 16, <http://www.thecitizen.co.tz/News/> (imesomwa 25-7-2017).
- Khamis, Bakari Z. 2019. Nyimbo za Wasanii wa Kike wa Bongofleva Zinavyoendeleza Maudhui ya Kimfumodume Nchini Tanzania. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kipacha, Ahmad. 2014. Misemo katika Lugha za Magari: Divai Mpya? *Swahili Forum* 21:104-121.
- King'ei, Kitula & Ahmed Ndal. 2009. *Kamusi ya Methali*. Nairobi: East African Educational Publishers.

## METHALI ZA KISWAHILI ZIHUSUZO ULEMAVU

- Kisanji, Joseph. 1995. Attitudes and beliefs about disability in Tanzania. *Innovations in Developing Countries for People with Disabilities*, ed. by Brian O'Toole & Roy McConkey. Chorley: Li sieux Hall Publications. Pp. 51-70.
- Kiyaga, Nassozi B & Moores, Donald F. 2003. Deafness in Sub-Saharan Africa. *American Annals of the Deaf* 148,1: 18-24.
- Kristensen, Kirsten, Martin Omagor-Loican & Negriz Onen. 2003. The Inclusion of Learners with Barriers to Learning and Development into Ordinary School Settings: A Challenge for Uganda. *British Journal of Special Education* 30:194-201.
- Madafa, Emanuel. 2016. Mtoto agundulika akiwa amefungiwa ndani na wazazi wake kwa miaka 11 mkoani Mbeya. <http://issamichuzi.blogspot.com/2016/07/mtoto-agundulika-akiwa-amefungiwa-ndani.html> (imesomwa tarehe 13-7-2016).
- Madumulla, Joshua S. 2009. *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.
- Mahenge, Elizabeth G. 2013a. *Fasihi na Ulemavu: Uchambuzi wa Methali za Kiswahili*. London: Lulu.com.
- Mahenge, Elizabeth G. 2013b. Msigano wa Majina ya 'Walemavu' katika Jamii ya Wazungumzaji Kiswahili: Mifano kutoka Tanzania. *Kioo cha Lugha* 11: 78-89.
- Mahenge, Elizabeth G. 2019. *Uumbaji wa Ualbino katika Fasihi ya Kiswahili: Uchambuzi wa Kazi Teule*. Tasinifu ya PhD (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Matei, Assumpta K. 2011. *Fani ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mbiti, John. 1975. *Introduction to African Religions* (2<sup>nd</sup> ed.). Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Mbiti, John. 2011. *African Religions and Philosophy*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Mbughuni, Patricia. 1982. The Image of Women in Kiswahili Prose Fiction. *Kiswahili* 49,1: 15-24.
- Mieder, Wolfgang. 1997. Modern Paremiology in Retrospect and Prospect. *Paremia* 6: 399-416.
- Milton, Derick. 2017. Wanaume Wadaiwa Kukimbia Familia Wakipata Watoto Albino. *Mtanzania*. 18 Machi 2017, uk 8.
- MLYDS. 2004. *National Policy on Disability*. Dar es Salaam: MLYDS.



SHANI OMARI MCHEPANGE & ELIZABETH GODWIN MAHENGE

- Momanyi, Clara. 2001. Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaban Robert. *Kiswahili* 64: 53-63.
- Momoh, Campbell S. 2000. *Philosophy in African Proverbs*. Auch: African Philosophy Projects Publications.
- Mrikaria, Steven. Kamusi ya Methali za Kiswahili. Haijachapishwa.
- Msokile, Mbunda. 1993. *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Muhando, Penina. 1982. *Nguzo Mama*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mulokozi, Mugyabuso & Shani Kitogo (wah.) 2007. *Mithali na Mifano ya Kiswahili - Shaaban Robert*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mulokozi, Mulokozi K. 2018. Tazunguzi za Fasihi Simulizi, *Mulika* 21: 1-24.
- Mung'ong'o, Claude G. 1980. *Njozi Iliyopotea*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mushumbusi, Raymond. 2016. Watu wenye Ulemavu Wajengewe Miundombinu Rafiki Kupunguza Changamoto za Kimaisha. <http://michuzi-matukio.blogspot.com/2016/05/watu-wenye-ulemavu-wajengewe.html>. (ilisomwa 16-5-2016).
- Nixon, Robert. 1985. Reception Theory and African Oral Literature: The Question of Performance. *English in Africa* 12,2: 53-61.
- Oladipo, Olusegun (ed.) 2002. *The Third Way in African Philosophy*. Ibadan: Hope Publications.
- Olaiya, Kolawole. 2013. Commodifying the "Sacred," Beatifying the "Abnormal": Nollywood and the Representation of Disability. *The Global South* 7,1: 137-156.
- Omari, Shani. 2008. Fasihi Simulizi na Jinsia: Mifano kutoka Nyimbo za Watoto Tanzania. *Kiswahili* 71: 98-115.
- Omari, Shani 2016. Swahili Modern Proverbs: The Role of Literary Writers and Blog Users, *Swahili Forum* 23: 21-46.
- Oriedo, Hannington E. 2007. *Istilahi za Fasihi ya Kiswahili*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Oruka, Henry Odera. 1983. Sagacity in African Philosophy. *International Philosophical Quarterly* 23,4: 383-393.
- Quayson, Ato. 2003. *Calibrations: Reading for the Social*. Minneapolis: University of Minnesota Press.

## METHALI ZA KISWAHILI ZIHUSUZO ULEMAVU

- Reeve, Donna. 2002. Negotiating Psycho-emotional Dimensions of Disability and their Influence on Identity Constructions. *Disability and Society* 17,5: 493–508.
- Reeve, Donna. 2006. Towards a Psychology of Disability: The Emotional Effects of Living in a Disabling Society. *Disability and Psychology: Critical Introductions and Reflections*, ed. by Dan Goodley and Rebecca Lawthom. Basingstoke: Palgrave Macmillan. Pp. 94-107.
- Rosenblatt, Louise M. 1969. Towards a Transactional Theory of Reading. *Journal of Literacy Research* 1: 31-49.
- Rutachwamagyo, Kaganzi. 2000. *Dhana ya Elimu Jumuishi: Ulemavu na Haki ya Elimu nchini Tanzania*. Dar es Salaam: Kituo cha Habari kuhusu Ulemavu.
- Senkoro, Fikeni E.M.K. 2011. *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Stone-MacDonald, Angi. 2012. Preparing Children with Developmental Disabilities for Life in the Community: A Tanzanian Perspective. *Education and Training in Autism and Developmental Disabilities* 47,3: 255-268.
- Teferra, Tirussew. 1994. Psychosocial and educational profile of students with disabilities in Addis Ababa University. *The Ethiopian Journal of Health Development* 8,1: 43-61.
- Teklu, Abebe A. 2010. We Cannot Clap with One Hand: Global Socio–Political Differences in Social Support for People with Visual Impairment. *International Journal of Ethiopian Studies* 5,1: 93-105.
- Tempels, Placide. 1959. *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.
- Thomas, Carol. 2004. How is Disability Understood? An Examination of Sociological Approaches. *Disability & Society* 19,6: 569-583.
- Thompson, Martyn P. 1993. Reception Theory and the Interpretation of Historical Meaning. *History and Theory* 32,3: 248-272.
- TUKI 2014. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Tatu). Nairobi: Oxford University Press.
- UN 2006. ‘United Nations Convention on the Rights of Persons with Disabilities’ [https://www.un.org/disabilities/documents/convention/convention\\_accessible\\_pdf.pdf](https://www.un.org/disabilities/documents/convention/convention_accessible_pdf.pdf)
- UN 2019. ‘A double challenge for the disabled’ <https://www.un.org/africarenewal/magazine/december-2018-march-2019/double-challenge-disabled/>
- Van Campen, Cretien & Marc Van Santvoort. 2013. Explaining Low Subjective Well-Being of Persons with Disabilities in Europe: The Impact of Disability, Personal Resources,

Participation and Socio-Economic Status. *Social Indicators Research: An International and Interdisciplinary Journal for Quality-of-Life Measurement* 111,3: 839-854.

Wafula, Richard & Njogu, Kimani. 2007. *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, Kyallo W. 2002. *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, Kyallo W. 2010. *Kamusi ya Methali*. Nairobi: Longhorn Publishers.

WHO 2021. 'Disability and health' <https://www.who.int/news-room/fact-sheets/detail/disability-and-health>

Yankah, Kwesi. 1999. Proverb. *Journal of Linguistic Anthropology* 9,1/2: 205-207.

### **Kiambatisho: Methali zaidi kuhusu ulemavu**

1. Alipo kilema usikunje kidole (Mrikaria h.t:38)
2. Bibi mzuri hakosi kilema (Wamitila 2010: 293, King'ei & Ndalu 2009:253, Mrikaria h.t:71)
3. Chongo huwa mfalme wa vipofu (Wamitila 2010:359).  
Chongo ni mfalme wa vipofu (King'ei & Ndalu 2009:327)
4. Chozi la akupendaye hutoka kwenye chongo (King'ei & Ndalu 2009:331, Wamitila 2010:362)
5. Elimu kidogo wazimu (Robert 2007:280)
6. Fadhaa hutia kichaa (Robert 2007:292)
7. Hujui kula na kipofu usingemgusa vyanda (Wamitila 2010:560)  
Hujui kula na kipofu usingemgusa mkono (King'ei & Ndalu 2009:573)
8. Kilema cha kutafuta hakipewi pole (Mrikaria h.t:29)
9. Maafuu hapatilizwi (maafuu ni mtu aliyeharibikiwa na akili) (Wamitila 2010:933, King'ei & Ndalu 2009:1020).
10. Mgeni pofu ingawa ana macho yake (Wamitila 2010:1122).  
Mgeni kipofu ingawa macho anayo (King'ei & Ndalu 2009:1246)  
Mgeni ni kipofu (Mrikaria h.t:189)

## METHALI ZA KISWAHILI ZIHUSUZO ULEMAVU

11. Mpofuka ukongweni hapotewi na njia (Wamitila 2010:1246, King'ei & Ndalul 2009:1403).
12. Mtu ambaye anamdhihaki kiwete au mlemavu inambidi awe mzima au kamili (Mrikaria h.t:213)
13. Mungu akikupa kilema atakuonya na mwendo wake (King'ei & Ndalul 2009:1553).  
Mtukana kilema hakimu ni Mungu (King'ei & Ndalul 2009:1531).
14. Mwenye kibyongo halali tani (Wamitila 2010:1454, King'ei & Ndalul 2009:1657, Mrikaria h.t:225).
15. Mwenye kushiriki moyo asorudi mtima, hufa maji pondo-ima, na kuondoka na kilema (Wamitila 2010:1466, King'ei & Ndalul 2009:1670).
16. Penye vipofu wengi kengeza hufaidi (Wamitila 2010:1686, King'ei & Ndalul 2009: 1932).
17. Pofu hasahau gongole (mkongojo wake) (Wamitila 2010:1862).  
Pofu hasahau mkongojo wake (King'ei & Ndalul 2009:1944)
18. Si vema kucheka kilema (Robert 2007:1232)
19. Ukila na kipofu usimguse mkono (Mrikaria h.t:276)
20. Ukienda kwa wenye chongo, vunja lako jicho (King'ei & Ndalul 2009:2160)
21. Ukienda kwa wenye chongo fumba lako jicho (Wamitila 2010:1862).
22. Ukikaa mjini mwa wenye chongo, nawe vunja lako jicho (Robert 2007:1294)
23. Ukipofuka na utu uzima pawekwapo chumvi wapajua (Robert 2007:1307)
24. Usile na kipofu ukamgusa mkono (Mrikaria, h.t:288, Wamitila 2010:1988)
25. Wanja wa manga si dawa ya chongo (Wamitila 2010:2085).